



Fomu ya Idhini ya Maelezo ya Uchunguzi wa Maiti kwa Patholojia ya Tishu ya RECOVER



RECOVER

Researching COVID to Enhance Recovery

An Initiative Funded by the National Institutes of Health

RECOVERcovid.org

Asante kwa nia yako ya kushiriki katika Utafiti wa RECOVER.

Pole sana kwa kifo cha mpendwa wako. Kwa kujiunga na utafiti wa RECOVER, mpendwa wako anaweza kutusaidia kujifunza kuhusu athari za kudumu za COVID kwenye afya kwa njia ambazo haziwezekani ikiwa angekuwa hai.



Uchunguzi wa Maiti ni nini?

Uchunguzi wa maiti ni uchunguzi wa kimatibabu unaofanyiwa mwili baada ya kufariki. Hospitalini, daktari (anayeitwa mwanapatholojia) anafanya uchunguzi wa maiti ili kujifunza mengi zaidi kuhusu jinsi mtu alivyofariki na kilicho sababisha kifo hicho.

Mbona chunguzi za maiti hufanywa?

Uchunguzi wa maiti unaweza kutusaidia kuelewa kilichosababisha kifo na kujua kama mtu huyo alikuwa na magonjwa fulani.

Kwa nini RECOVER wanafanya utafiti wa uchunguzi wa maiti (pia unaitwa utafiti wa patholojia ya tishu)?

Katika utafiti huu, tunataka kuelewa kwa nini baadhi ya watu wanaokumbwa na COVID wanapata nafuu, ilhali watu wengine wanasalia wagonjwa kwa muda mrefu. Kama sehemu ya utafiti wa RECOVER, watafiti wanafanya uchunguzi wa maiti kwa mtu aliyefariki ili kujua yafuatayo:

- Jinsi COVID inavyoathiri sehemu tofauti za mwili
- Athari za kudumu za COVID

Pia watafiti watapitia maelezo yaliyo kwenye rekodi za afya za mtu aliyefariki.

Ni nini hufanyika wakati wa uchunguzi wa maiti?

Daktari (anayeitwa mwanapatholojia) anatazama nje na ndani ya mwili baada ya kifo. Wanakusanya sampuli ndogo za tishu na viungo vya mwili ili kuvitafiti, kama vile:

- Damu au majimaji mengine, kama vile maji ya uti wa mgongo
- Macho
- Ubongo
- Moyo
- Mapafu
- Ini
- Wengu
- Kongosho
- Figo
- Kibofu cha mkojo
- Viungo vilivyo tumboni, kama vile matumbo au utumbo

Unaweza kuchagua kuwaruhusu watazame tu sehemu fulani za mwili (kwa mfano, kuanzia tu kifua na tumbo, si kichwa). Lakini, hili linaweza kuifanya kuwa vigumu kujua kilichosababisha kifo na inaweza kufanya uchunguzi huo wa maiti kutokuwa wa manufaa kwa utafiti wa RECOVER.

Ni nini hufanyika baada ya uchunguzi wa maiti?

Kama sehemu ya zoezi za utafiti:

- 1 Sampuli zinazohitajika kwa utafiti zitapatiwa nambari ya kipekee na mwanapatholojia, kwa hivyo hazitakuwa na maelezo yoyote yanayomtambulisha mtu kibinafsi.
- 2 Kisha kwa uangalifu na heshima wanautayarisha mwili ili kuwezesha watu kuuona mwili wakati wa mazishi, au tukio lingine ambapo mwili unaweza kutazamwa.
- 3 Watatuma sampuli hizo hadi maabarani kuhifadhiwa (inaitwa hifadhi ya kibayolojia) ili kufanyiwa vipimo baadaye.





Nitapata matokea yanayotokana na uchunguzi wa maiti?

Unaweza kupata ripoti ya matokeo ya uchunguzi wa maiti, ikiwa wewe ndiye mrithi wake kisheria.



Mwanapatholojia ataandika ripoti kuhusu alichojifunza kutokana na uchunguzi wa maiti, ambao utajumuisha kilichosababisha kifo, ikiwa inajulikana.

Kwa kawaida ripoti zinapatikana ndani ya siku 60 za kazi, ingawa baadhi ya ripoti huenda zikachukuwa muda mrefu zaidi.



Tunahamasisha sana kwamba upitie ripoti hii pamoja na daktari wako ambaye anaweza kukusaidia kuelezea matokeo.

Ripoti haitajumuisha matokeo ya utafiti kutoka kwa utafiti wa RECOVER, kama vile maelezo kuhusu jeni (sehemu ya DNA inayopitishwa kutoka kwa mzazi hadi mtoto ambayo huambia seli cha kufanya).

Maelezo yanayotokana na uchunguzi wa maiti yatawekwa faraghani (kwa siri)?



Ndiyo, kila kitu kinachotokana na uchunguzi wa maiti kitawekwa faraghani, kumaanisha kwamba ni watu tu walio na ruhusa wanaweza kuona maelezo kuhusu uchunguzi wa maiti.

Watu wanaoweza kuona maelezo wanajumuisha:

- Madaktari waliomhudumia mtu huyo
- Wanapatholojia wanaofanya uchunguzi wa maiti au wanaotazama sampuli
- Wato huduma wa afya wengine waliohitimu
- Timu ya zoezi la utafiti wa RECOVER – watafiti wakizungumza kuhusu au kuandika majarida ili kushiriki walichojifunza katika utafiti huu, hawatajumuisha maelezo yoyote yanayoweza kuwatambulisha watu waliofariki na walikuwa sehemu ya utafiti huu

Nitahitajika kulipia uchunguzi wa maiti?

La. Hakutakuwa na gharama kwako wala kwa familia yako kwa ajili ya uchunguzi wa maiti.

Tupo hapa kujibu maswali yako kuhusu kuruhusu mpendwa wako aliyefariki kushiriki katika utafiti wa RECOVER.

Tutumie maswali yako kwa kupitia barua pepe kwa anwani:

RECOVER_Tissue_Pathology@nyulangone.org



Au skani msimbo huu wa QR ukitumia simu yako ili upate barua pepe iliyojazwa mada na ujumbe kwenye programu yako ya barua pepe.

Ili kupata maelezo zaidi kuhusu utafiti wa RECOVER, tembelea:

RECOVERcovid.org